Nyaraka Na.: TFDA/DMC/CCM/G/005

MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA

MWONGOZO WA KUTAMBUA NA KUSAJILI MAJENGO YANAYOJIHUSISHA NA BIASHARA YA VIPODOZI

Umeandaliwa kwa mujibu wa Kanuni za Udhibiti wa Vipodozi za mwaka 2010

Toleo la Kwanza

Novemba 2017

Barabara ya Mandela, Mabibo External, S.L.P 77150, Dar es Salaam - Tanzania
Simu ya mezani: +255 22 2450512/2450751/2452108
Simu ya mkononi: +255 658 445222/685 701735/777 700002
Nukushi: +255 222450793
Tovuti: www.tfda.go.tz, Barua Pepe: info@tfda.go.tz
Simu ya kupiga bure: 0800110084

YALIYOMO

SHUKRANI 3
DIBAJI 4
UTANGULIZI 5
TAFSIRI YA MANENO 6
SEHEMU YA KWANZA: MAELEZO YA JUMLA 8
SEHEMU YA PILI: UTAMBUZI 9
SEHEMU YA TATU: USAJILI WA MAJENGO YA BIASHARA 10
SEHEMU YA NNE: VIGEZO VYA USAJILI WA MAJENGO 12
SEHEMU YA TANO: USAJILI WA VIPODOZI 17
SEHEMU YA SITA: MGAWANYO WA MAJUKUMU 18
SEHEMU YA SABA: UENDESHAJI WA BIASHARA YA VIPODOZI 19
SEHEMU YA NANE: VIAMBATISHO 23

SHUKRANI

Mwongozo huu wa kutambua na kusajili majengo yanayojihusisha na biashara ya vipodozi umeandaliwa kwa mara ya kwanza na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA). Uandaaji wa mwongozo huu umelenga kuwasaidia wafanyabiashara pamoja na wajasiriamali wadogo wanaofanya biashara ya vipodozi kwenye soko la Tanzania kuweza kufahamu taratibu za usajili wa majengo yao na uendeshaji wa biashara kwa ujumla.

TFDA inaishukuru timu ya wataalam walioainishwa hapa chini kwa kuandaa rasimu ya kwanza ya mwongozo huu:

a. Bw. Joseph H. Nziku - Shirika la Viwango Tanzania
b. Bi. Halima Kazindogo - Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo
c. Bi. Grace M. Shimwela - Mamlaka ya Chakula na Dawa
d. Bi. Gudula Mpanda - Mamlaka ya Chakula na Dawa
e. Bi. Gloria Matemu - Mamlaka ya Chakula na Dawa
f. Bw. Maganga Bundala - Mamlaka ya Chakula na Dawa
g. Bw. Seth Kisenge - Mamlaka ya Chakula na Dawa

Wadau waliotoa maoni yao katika kuboresha mwongozo tajwa pia wanashukuriwa ikiwa ni pamoja na Menejimenti ya TFDA kwa kuidhinisha matumizi yake.

Adam Mitangu Fimbo
Mkurugenzi, Dawa na Bidhaa Nyongeza
Mamlaka ya Chakula na Dawa

DIBAJI

Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) ni Wakala wa Serikali chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto iliyoanzishwa mwaka 2003 kwa lengo la kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa chakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi. TFDA inatekeleza majukumu yake chini ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sura 219. Sheria hii inakataza utengenezaji, usambazaji na uuzaji wa bidhaa zinazodhibitiwa ikiwemo vipodozi bila ya vibali au leseni zinazotolewa na TFDA.

TFDA imekuwa ikisajili na kutoa leseni kwa majengo mbalimbali tangu mwaka 2003. Hata hivyo kumekuwa na changamoto mbalimbali kwa upande wa wajasiriamali wadogo wa vipodozi katika kutekeleza matakwa ya Sheria hususan suala la usajili na utoaji wa leseni za kuendesha biashara. Baadhi ya changamoto hizo ni: -

a) Uwepo wa wazalishaji na wauzaji wadogo katika maeneo yasiyo rasmi na yasiyokidhi mahitaji ya Sheria kama vile maeneo ya makazi au majumbani, vyombo vya usafiri, minada, mitandao ya kijamii, mitaani na kwenye maonesho ya kibiashara.
b) Wazalishaji wadogo kutokidhi mahitaji ya miongozo ya usajili na utengenezaji bora wa vipodozi.
c) Wajasiriamali wadogo kuwa na uelewa mdogo wa lugha ya kiingereza iliyotumika kwenye miongozo mbalimbali.
d) Uelewa mdogo juu ya vipodozi kama sehemu ya bidhaa zinazodhibitiwa na TFDA.
e) Mitaji midogo ya wajasiriamali hivyo kufanya viwanda vyao kukosa sifa mfano mitambo duni na kushindwa kuweka maabara kwa ajili ya uchunguzi.
f) TFDA kutotambua wajasiriamali wote na maeneo waliko.

Kwa kuzingatia changamoto hizi na kwa kutambua umuhimu wa wajasiriamali katika kutengeneza ajira, kupunguza umaskini, kuongeza pato la taifa na kusaidia ukuaji wa sekta ya viwanda na teknolojia kama ilivyoainishwa kwenye *Sera ya Kuendeleza Wajasiriamali Wadogo na wa Kati (SMEs) ya mwaka 2003* ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, TFDA imeandaa mwongozo huu ili kurahisisha udhibiti na usimamizi wa biashara ya vipodozi nchini. Hatua hii itachangia katika kufikia lengo la kulinda afya ya jamii pamoja na maazimio ya Taifa ya uchumi wa kati na Tanzania ya viwanda.

Wajasiriamali wanaoendesha na wanaotarajia kuanzisha biashara ya vipodozi watapaswa kusoma mwongozo huu pamoja na Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sura 219 na Kanuni zake ili kufahamu taratibu za usajili wa maeneo yao na uendeshaji wa biashara ya vipodozi. Kama ilivyo desturi TFDA itaendelea kupokea maoni kutoka kwa wadau katika kuboresha matumizi ya mwongozo huu.

Hiiti B. Sillo
Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Chakula na Dawa

UTANGULIZI

Vipodozi ni miongoni mwa bidhaa zinazodhibitiwa na TFDA ambazo zimekuwa zikitumika kwenye maeneo mengi na kwa kiasi kikubwa. Hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la vipodozi vinavyoingizwa nchini na vile vinavyotengenezwa na viwanda vya ndani wakiwemo wajasiriamali wadogo. Utengenezaji wa vipodozi unahusisha viambata mbalimbali ambavyo iwapo havitawekwa kwa viwango sahihi na kwa usimamizi sahihi vinaweza kusababisha madhara kwa mtumiaji. Vile vile vipodozi vinapaswa kutunzwa na kusambazwa kwa usahihi ili viendelee kuwa na ubora na usalama unaokubalika.

Katika kuwezesha hili TFDA imeandaa mwongozo huu ili kuweza kuwatambua na kuwasajili wajasiriamali wanaojihusisha na biashara ya vipodozi hapa nchini kwa lengo la kurahisisha udhibiti na usimamizi. Mwongozo umegawanywa katika sehemu nane ambapo sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya jumla, sehemu ya pili inaainisha namna ambavyo wajasiriamali watatambuliwa, sehemu ya tatu inaelekeza utaratibu wa usajili wa majengo ya biashara na sehemu ya nne inatoa vigezo vya usajili wa majengo. Vile vile sehemu ya tano inafafanua utaratibu wa kusajili vipodozi, sehemu ya sita inaainisha mgawanyo wa majukumu, sehemu ya saba inaelekeza namna ambavyo biashara ya vipodozi itaendeshwa na sehemu ya nane ni fomu mbalimbali za utumaji wa taarifa za kuwezesha tathmini na utoaji wa vibali au leseni za biashara.

Mwongozo utawezesha kuwatambua wajasiriamali ambao wamekuwa wakifanya biashara ya vipodozi kwenye maeneo mbalimbali bila ya kufahamika na kuleta changamoto kwenye udhibiti. Wale wote wenye nia ya kuanzisha biashara ya utengenezaji, uuzaji wa jumla na rejareja, maghala na magari ya kubebea vipodozi watapaswa kufuata masharti yaliyowekwa kwenye mwongozo wakati wa kuwasilisha maombi ya usajili wa majengo yao na vibali. Pamoja na mwongozo huu watengenezaji wakubwa na wa kati wa vipodozi watapaswa pia kutimiza vigezo vilivyoainishwa kwenye Mwongozo wa Utengenezaji Bora wa Vipodozi (Good Manufacturing Practices Guidelines for Cosmetics) wa mwaka 2015.

Aidha, wadau wengine kama SIDO, VETA, TBS na wakaguzi wa TFDA wanaweza kutumia mwongozo huu kutoa elimu kwa wajasiriamali na wakati wa kutekeleza majukumu kwenye maeneo yao ya kazi.

TAFSIRI YA MANENO

Kwa mujibu wa mwongozo huu, maneno yametafsiriwa kama ifuatavyo:-

BRELA: Ni wakala wa Serikali ulioanzishwa chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Sheria ya Wakala wa Serikali Na. 3 ya mwaka 1997 kwa lengo la kusajili Biashara na Leseni.

Duka la jumla: ni duka linalouza vipodozi kwa maduka mengine kwa lengo la kuuza rejareja.

Duka la rejareja: Ni duka linalouza vipodozi kwa mtumiaji wa mwisho.

Eneo: Inajumuisha ardhi, jengo au sehemu yoyote ya jengo kwa ajili ya kutengeneza, kuuza au kuhifadhi vipodozi au chombo maalum cha kusafirisha vipodozi.

Ghala: Ni jengo linalotumika kuhifadhi vipodozi kwa ajili ya kuuzwa.

Kanuni: Ni taratibu zilizoandaliwa na waziri mwenye dhamana kutokana na Sheria na zina nguvu ya kimahakama.

Kiambato: Ni kitu chochote kinachoongezwa aidha peke yake au na kingine kama sehemu ya kipodozi.

Kipodozi au vipodozi: Ni kitu chochote kinachoweza kutumika kwenye mwili au sehemu ya mwili kwa njia ya kupaka, kuosha, kunyunyizia, kufukiza au kupulizia kwa ajili ya kusafisha, kujiremba, kujipamba au kuongeza uzuri wa ngozi au kubadili muonekano wa sura. Aidha, kipodozi au vipodozi hakipaswi kuonesha kuwa kinatibu au kupunguza maambukizi ya magonjwa.

Kipukusi au Vipukusi: Ni dawa iliyo katika mfumo wa kimiminika ambayo hutumika kuua vijidudu vinavyoweza kusababisha maambukizi.

Minada/Gulio/Masoko: Ni eneo maalum lililotengwa na kumilikiwa na Halmashauri ya Mji au Serikali ya kijiji/mtaa kwa ajili ya wafanyabiashara kununua au kuuza mazao ya chakula na biashara na hata bidhaa za viwandani mfano vipodozi.

Mwongozo: Ni taratibu zilizowekwa ili kusaidia utendaji.

Rasimisha: Ni kuwatambua au kuwasajili wajasiriamali wa vipodozi kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa sambamba na kuweka orodha yao kwenye tovuti ya TFDA.

Sheria: Ni taratibu zilizowekwa na bunge na zina nguvu ya kimahakama; kwa mujibu wa mwongozo huu Sheria inamaanisha Sheria ya Chakula, Dawa na vipodozi, Sura 219.

SIDO: Ni shirika la kuhudumia viwanda vidogo lililoanzishwa kwa Sheria ya Bunge No. 28 ya mwaka 1973 chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa lengo la kupanga, kuratibu, kuhamasisha na kujenga uwezo wa wajasiriamali wadogo.

TBS: Ni shirika la umma chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji lililoanzishwa kwa Sheria ya Viwango Na. 2 ya mwaka 2009 likiwa na jukumu la kuandaa viwango vya kitaifa na kusimamia utekelezaji wake.

Uchuuzi: Ni biashara ndogondogo inayohusisha kuuza vipodozi kwa kutembea kutoka sehemu moja au nyingine au katika eneo lisilo rasmi na lisilo la kudumu.

Utengenezaji: Ni shughuli zote katika uzalishaji, maandalizi, mchakato, upakiaji, ubadilishaji, upakiaji upya na uwekaji lebo wa bidhaa za vipodozi.

Wajasiriamali: Ni wafanyabiashara wanaojihusisha na utengenezaji au uuzaji wa vipodozi.

Wauzaji: Ni wajasiriamali ambao hawajihusishi na utengenezaji wa vipodozi, kazi yao ni kununua vipodozi kutoka maduka ya jumla au watengenezaji na kuviuza kwa jumla au rejareja.

Watengenezaji wadogo/viwanda vidogo: Ni wajasiriamali wanaojihusisha na uzalishaji wa vipodozi ambao mtaji wao wa mitambo na vifaa hauzidi shilingi milioni mia mbili (200) na idadi ya watumishi haizidi arobaini na tisa (49). Ni viwanda vinavyotengeneza vipodozi visivyozidi 100 kutegemeana na aina (mfano lita 100, vipande 100, miche 100 nk.) kwa toleo moja.

VETA: Ni Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bunge Namba 1 ya mwaka 1994 ikiwa na jukumu la kuratibu, kusimamia, kuwezesha, kukuza na kutoa elimu ya ufundi na mafunzo Tanzania.

SEHEMU YA KWANZA: MAELEZO YA JUMLA

1.1 Wajasiriamali wa vipodozi wamegawanyika katika makundi manne (4) kwa kuzingatia idadi ya wafanyakazi na kiasi cha mtaji uliowekezwa katika biashara kama ilivyoainishawa kwenye *Sera ya Kuendeleza Wajasiriamali ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ya mwaka 2003*. Jedwali namba 1 hapa chini linaonesha makundi hayo ya wajasiriamali.

1.2 Mtaji utahusisha gharama za mitambo na vifaa pekee na hautahusisha ardhi, eneo au jengo.

Jedwali Namba 1: makundi ya wajasiriamali wa vipodozi

Kundi	**Idadi ya wafanyakazi**	**Mtaji (kwa shilingi)**
wadogo sana	1 hadi 4	mpaka milioni 5
wadogo	5 hadi 49	zaidi ya milioni 5 hadi 200
wa kati	50 hadi 99	zaidi ya milioni 200 hadi 800
wakubwa	zaidi ya100	zaidi ya milioni 800

1.3 Kwa mujibu wa mwongozo huu wajasiriamali ni watengenezaji wa vipodozi walio katika kundi la wajasiriamali wadogo sana (micro) na wajasiriamali wadogo (small) pamoja na wauzaji wa vipodozi ambao ni maduka ya jumla na rejareja, maghala na magari ya kubebea vipodozi.

1.4 Watengenezaji wa vipodozi walio katika kundi la kati na wakubwa watafuata masharti yaliyoainishwa kwenye kwenye Mwongozo wa Utengenezaji Bora wa Vipodozi (*Good Manufacturing Practice Guidelines for Cosmetics*).

1.5 TFDA itatumua vigezo vyote viwili kama ilivyoainishwa kwenye 1.1 hapo juu kugawa wajasiriamali katika makundi yaliyoainishwa kwenye mwongozo huu.

1.6 Mjasiriamali ni lazima awe raia wa Tanzania.

1.7 Wajasiriamali watapaswa kufuata taratibu zote zilizoainishwa kwenye mwongozo huu ikiwa ni pamoja na kuhakikisha vipodozi wanavyotengeneza au kuuza vinakidhi vigezo vya ubora na usalama.

1.8 Kutakuwa na njia tatu (3) za kurasimisha wajasiriamali wa vipodozi:-

a) Kwa njia ya utambuzi
b) Kwa njia ya kusajili maeneo ya biashara (mfano watengenezaji, wauzaji, maghala n.k).
c) Kwa njia ya usajili wa vipodozi.

1.9 Mjasiriamali anapaswa kuwasilisha taarifa sahihi na za kweli kuhusiana na biashara au bidhaa anayokusudia kutengeneza au kuuza.

1.10 Taarifa zitawasilishwa kwa lugha ya kiswahili au kiingereza pale itakapowezekana.

1.11 Ni kosa kutengeneza, kuuza au kusambaza vipodozi pasipo kuwa na kibali, usajili au kutambuliwa na TFDA.

1.12 Ni kosa pia kutangaza vipodozi kwa njia yoyote ile ikiwemo kwenye mitandao pasipo kuwa na kibali kutoka TFDA.

SEHEMU YA PILI: UTAMBUZI

2.1 Utambuzi maana yake ni kumfahamu mjasiriamali anayejihusisha na biashara ya utengenezaji, usambazaji au uuzaji wa vipodozi nchini bila ya usajili kutoka TFDA.

2.2 Utambuzi utahusisha kubaini au kuainisha eneo la biashara, aina ya biashara (mfano kutengeneza, kuuza au kuhifadhi), aina ya vipodozi na mmiliki wa biashara.

2.3 TFDA kupitia ofisi za kanda itafanya utambuzi wa wajasiriamali wanaojihusisha na biashara za vipodozi.

2.4 Jinsi ya kufanya utambuzi

2.4.1 Mjasiriamali atajaza fomu (Kiambatisho 1) ya kujitambulisha na kuiwasilisha kwenye ofisi ya kanda husika.

2.4.2 TFDA kupitia ofisi za kanda itafanya ukaguzi kuhakiki taarifa zilizowasilishwa na kutoa maelekezo sahihi pale itakapobidi.

2.4.3 Mjasiriamali atapewa barua ya kutambuliwa baada ya uhakiki wa taarifa zake.

2.4.4 Mjasiriamali aliyetambuliwa atatakiwa kusajili eneo la biashara katika kipindi kitakachoainishwa na TFDA.

2.4.5 Ofisi za kanda zitatunza kumbukumbu za wajasiriamali waliotambuliwa.

2.4.6 Kumbukumbu zitaainisha jina la biashara, mmiliki wa biashara, aina ya biashara, eneo la biashara, majina na aina ya vipodozi vinavyotengenezwa au kuuzwa. Kumbukumbu zitaainisha pia kundi sahihi la mjasiriamali (mfano kiwanda kidogo sana, kiwanda kidogo, duka la jumla, duka la reja reja, duka la jumla na rejareja, ghala n.k).

2.4.7 Orodha ya wajasiriamali waliotambuliwa itawekwa kwenye tovuti ya TFDA (www.tfda.go.tz) na njia nyingine za mawasiliano.

2.5 Ofisi za kanda zitatoa elimu kwa wajasiriamali waliotambuliwa ili waweze kufikia vigezo vya kusajili maeneo yao ya biashara pamoja na vipodozi ambavyo havijasajiliwa.

2.6 TFDA kupitia ofisi za kanda inaweza kuwasiliana na taasisi zinazojihusisha na mafunzo ya wajasiriamali mfano SIDO au VETA kupata taarifa za wajasiriamali wa vipodozi ambao bado hawajatambuliwa.

2.7 Wajasiriamali ambao hawatawasilisha fomu za utambuzi wa maeneo yao ya biashara hawataruhusiwa kufanya biashara katika soko la Tanzania.

SEHEMU YA TATU: USAJILI WA MAJENGO YA BIASHARA

3.1 Maeneo ya biashara ya vipodozi yapo katika makundi mbalimbali kama ifuatavyo:-

3.1.1 Viwanda vidogo.

3.1.2 Maduka ya jumla na rejareja.

3.1.3 Maghala na magari ya kusafirishia.

3.1.4 Majumbani/ Makazi ya watu yanayotumika kutengeneza vipodozi.

3.1.5 Wachuuzi wa vipodozi kwenye mitaa.

3.1.6 Wauzaji kwa njia ya mitandao.

3.1.7 Wauzaji kwenye magari binafsi na mabasi.

3.1.8 Minada na maonesho mbalimbali ya kibiashara.

3.1.9 Viwanda vya kati na vikubwa.

3.2 Usajili wa viwanda vidogo vilivyoainishwa kwenye 3.1.1, waombaji watapaswa kufuata utaratibu ufuatao:-

3.2.1 Kujaza kwa ukamilifu fomu ya maombi ya kusajili jengo (Kiambatisho 2) na fomu ya maombi ya kibali au leseni (Kiambatisho 3) na kuwasilisha ofisi ya kanda husika.

3.2.2 Kulipia ada ya usajili wa eneo na kibali kwa mujibu wa kanuni za ada na tozo zinazotumika.

3.2.3 Baada ya kupokea fomu, TFDA itafanya ukaguzi wa eneo kwa kutumia fomu maalum (Kiambatisho 4) na endapo litakidhi, mwombaji atapewa cheti cha usajili wa eneo (Kiambatisho 5). Vigezo vya usajili wa maeneo vimeainishwa kwenye sehemu ya nne ya mwongozo huu.

3.2.4 Mwombaji atapewa muda zaidi wa kufanya ukarabati wa eneo endapo litaonekana kutokukidhi baadhi ya vigezo. Baada ya marekebisho mwombaji atawasilisha taarifa ya maandishi TFDA kwa ajili ya ukaguzi wa marudio.

3.2.5 Kibali au leseni (Kiambatisho 6) kitatolewa baada ya mwombaji kuwasilisha maombi ya usajili na vipodozi kusajiliwa.

Hivyo, baada ya kupewa cheti cha usajili wa jengo mmiliki atatakiwa kabla ya kupewa kibali au leseni ya kutengeneza vipodozi kuwasilisha sampuli pamoja na maombi ya usajili wa kipodozi/ vipodozi husika kwa kuzingatia mwongozo wa usajili wa vipodozi.

3.3 Usajili wa maeneo yaliyoainishwa kwenye 3.1.2 na 3.1.3, waombaji watapaswa kufuata utaratibu ufuatao:-

3.3.1 Kujaza kwa ukamilifu fomu ya maombi ya kusajili jengo (Kiambatisho 2) na fomu ya maombi ya kibali au leseni (Kiambatisho 3) na kuwasilisha ofisi ya kanda husika.

3.3.2 Kulipia ada ya usajili wa eneo na kibali kwa mujibu wa kanuni za ada na tozo zinazotumika.

3.3.3 Baada ya kupokea fomu, TFDA itafanya ukaguzi wa eneo kwa kutumia fomu maalum (Kiambatisho 7) na endapo litakidhi, mwombaji atapewa cheti cha usajili wa eneo (Kiambatisho 5) na kibali (Kiambatisho 6). Vigezo vya usajili wa maeneo vimeainishwa kwenye sehemu ya nne ya mwongozo huu.

3.3.4 Mwombaji atapewa muda zaidi wa kufanya ukarabati wa eneo endapo litaonekana kutokukidhi baadhi ya vigezo. Baada ya marekebisho mwombaji atawasilisha taarifa ya maandishi TFDA kwa ajili ya ukaguzi wa marudio.

3.4 Maeneo yaliyoainishwa kipengele 3.1.4 hadi 3.1.8 hayatasajiliwa na yataendelea kutambuliwa na TFDA kwa utaratibu ulioainishwa sehemu ya pili ya mwongozo huu.

3.5 Usajili wa viwanda vya kati na vikubwa kwenye 3.1.9 utafuata utaratibu ulioainishwa kwenye 3.2 isipokuwa litapaswa kukidhi vigezo vilivyoainishwa kwenye mwongozo wa utengenezaji bora wa vipodozi (*Good Manufacturing Practice Guidelines for Cosmetics*).

SEHEMU YA NNE: VIGEZO VYA USAJILI WA MAJENGO

4.1 Vigezo vya jengo kwa ajili ya kiwanda kidogo

4.1.1 Mahali

a) Jengo la kutengeneza vipodozi linapaswa kuwa katika maeneo safi na salama mbali na eneo linalotoa hewa, vumbi au moshi wenye sumu.

b) Ili kurahisisha ukaguzi na ufuatiliaji jengo liwe katika eneo linalofikika kwa urahisi. Mwombaji atatakiwa kuonesha namba ya simu na anwani ya eneo ambapo uzalishaji unafanyika ikionesha namba ya kiwanja, kitalu, namba ya nyumba, mtaa, kata, wilaya na mkoa pale itakapowezakana.

4.1.2 Muundo wa jengo

a) Jengo la kutengeneza vipodozi liwe imara na la kudumu.

b) Lisiwe na muingiliano wa moja kwa moja na biashara au makazi ambayo yatasababisha uchafuzi wa bidhaa zinazotengenezwa.

c) Liwe na nafasi ya kutosha ya kuwekea vifaa vya kuzalishia, kuhifadhi na kuchunguza malighafi na bidhaa zitakazotengenezwa na lenye kuruhusu kazi kufanyika kwa urahisi na mpangilio au mtiririko mzuri.

d) Liwe na mwanga na hewa ya kutosha kuruhusu shughuli za uzalishaji kufanyika kwa ufanisi bila ya kuathiri ubora wa malighafi na vipodozi vitakavyotengenezwa.

e) Liwe na vifaa vya kuzuia wanyama waharibifu kama panya, ndege, nyoka n.k kuingia kwenye jengo.

f) Lisiwe linavuja na liwe na kuta angavu, paa na sakafu zinazosafishika na kukarabatiwa kwa urahisi. Kuta na sakafu za ndani zipigwe plasta na kuwa nyororo. Zinaweza kuwa za vigae, terazo au saruji.

g) Liwe na rafu au chaga za kuhifadhia malighafi na vipodozi vilivyotengenezwa.

4.1.3 **Vifaa vya kutengeneza vipodozi**

a) Vifaa vya kutengeneza vipodozi viwe vya kutosha na vinavyokidhi mahitaji ya kazi husika.

b) Viwe vinasafishika, havishiki kutu, havichubuki wala kusababisha mabadiliko yeyote yasiyotakiwa kwenye vipodozi.

c) Visiwe na mikwaruzo ya kuweza kuhifadhi kemikali (mfano sabuni au *disinfectants*) au wadudu. Epuka vifaa au vyombo vilivyotengenezwa kwa shaba, risasi au chuma.

d) Viwe vinaruhusu usafi wa kutosha kufanyika kabla ya kuvitumia tena kuepuka uchafuzi wa vipodozi vinavyotengenezwa kutokana na mabaki ya bidhaa iliyopita. Visafishwe kabla na baada ya uzalishaji na viwe visafi wakati wote.

e) Endapo vipodozi vinavyozalishwa ni vya aina mbalimbali vifaa vioshwe kila baada ya kumaliza uzalishaji wa kipodozi cha aina moja ili kuepuka kuchafuana.

4.1.4 **Malighafi**

a) Malighafi zitakazotumika kutengenezea vipodozi zitoke katika vyanzo vinavyojulikana (kiwandani au dukani) na ziwe na nyaraka muhimu.

b) Malighafi zitunzwe katika hali ya usafi kwenye sehemu iliyotengwa na usiwepo uwezekano wa kuchanganyana.

c) Malighafi zitakazotumika ziwe ndani ya muda wake wa matumizi.

d) Epuka kutumia malighafi zenye viambato vilivyopigwa marufuku kutumika kwenye vipodozi.

e) Maji kwa ajili ya kutengeneza vipodozi yawe safi na salama kuepuka uchafuzi wa bidhaa itakayozalishwa.

4.1.5 **Wafanyakazi**

a) Kuwe na wafanyakazi wa kutosha kukidhi mahitaji ya kazi husika.

b) Kuwe na msimamizi wa shughuli zote za uzalishaji aliyepata mafunzo kutoka taasisi zinazotambuliwa na Serikali kama vile SIDO au VETA.

c) Mfanyakazi mwenye magonjwa ya kuambukiza asiruhusiwe kufanya kazi inayohusu kushika moja kwa moja bidhaa inayozalishwa.

d) Wafanyakazi wanaohusika moja kwa moja na uzalishaji watatakiwa kupewa mafunzo ya utengenezaji bora wa vipodozi na tahadhari za kuchukua ili kuepuka kuathiri ubora na usalama wa vipodozi vinavyozalishwa.

e) Wafanyakazi wanaohusika moja kwa moja na uzalishaji wavae mavazi maalum na vifaa vya kujikinga mfano mask, gloves.

f) Wafanyakazi wote lazima wawe wasafi na wasiwe na tabia zisizofaa kama kuvuta sigara, kupiga chafya na kukohoa bila kufunika kinywa, kulamba vidole au kujishika mwili wakati wa uzalishaji.

4.1.6 **Usafi wa mazingira**

a) Kuwe na choo/vyoo vya kutosha kwa ajili ya wafanyakazi. Endapo choo ni cha shimo kiwe mbali na jengo la uzalishaji upande ambapo hakiwezi kupeperusha upepo wenye hewa mbaya kwenda kwenye bidhaa inayozalishwa.

b) Kuwe na maji ya kutosha na sabuni kwa shughuli za uzalishaji na usafi kwa ujumla.

c) Kuwe na eneo maalum la kunawia mikono pamoja na sabuni au kipukusi.

d) Kuwe na utaratibu maalum wa kuhifadhi na kuharibu taka na usiwepo uwezekano wa kuchafua mazingira yanazunguka.

4.1.7 **Nyaraka na kumbukumbu**

a) Msimamizi wa shughuli za uzalishaji au mmiliki atatakiwa kuhakikisha uwepo wa nyaraka na kumbukumbu zifuatavyo:-

- Vyeti vya elimu na ujuzi wa wafanyakazi,
- Kumbukumbu za usafi,
- Kitabu cha kumbukumbu za manunuzi ya malighafi na mauzo ya vipodozi vilivyotengenezwa,
- Kitabu cha kumbukumbu za kaguzi,
- Taarifa za mafunzo kwa wafanyakazi,
- Taarifa za malalamiko juu ya ubora na usalama wa vipodozo vinavyotengenezwa,
- Kitabu cha kumbukumbu ya vipodozi visivyofaa/ vilivyorejeshwa kutoka kwenye soko kwa sababu fulani/vilivyofutiwa usajili,
- Kanuni na miongozo mbalimbali ya TFDA,
- Taarifa za utengenezaji wa vipodozi,
- Kumbukumbu za uchunguzi wa vipodozi.

4.2 **Vigezo vya majengo, maghala na magari kwa ajili ya kuuza, kuhifadhi na kusafirisha vipodozi**

4.2.1 **Maelezo ya jumla**

a) Maduka, maghala na magari ya kuuzia, kuhifadhi na kubebea vipodozi yanaweza kuuza, kuhifadhi au kubeba bidhaa nyingine zisizodhibitiwa na TFDA, isipokuwa vipodozi vitatakiwa kutengwa ili vibaki na ubora na usalama wake.

b) Maduka na maghala ya dawa yaliyosajiliwa chini ya *Sheria ya Famasi, Sura 311* yataruhusiwa kuuza na kuhifadhi vipodozi.

c) Maduka ya rejareja yanayojihusisha na biashara za chakula, vifaa tiba na vipodozi kwa wakati mmoja chini ya *Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sura 219* yatapewa kibali kimoja cha TFDA.

4.2.2 **Duka la kuuza vipodozi**

a) Duka la kuuza vipodozi linaweza kuwa duka la rejareja, duka la jumla au duka la jumla na rejareja kwa pamoja.

b) Duka la kuuzia vipodozi linapaswa kuwa katika mazingira safi na salama yasiyo hatarisha ubora wa vipodozi.

c) Duka liwe katika eneo linalofikika kwa urahisi ili kurahisisha ukaguzi na ufuatiliaji.

d) Duka liwe na muuzaji mwenye elimu isiyopungua kidato cha nne au aliyepitia mafunzo ya urembo kutoka katika vyuo vinavyotambuliwa na Serikali.

e) Duka la jumla au jumla na rejareja linaweza kuwa na ghala la kuhifadhia vipodozi ambalo litasajiliwa na TFDA kwa mujibu wa mwongozo huu.

f) Duka la kuuza vipodozi litapaswa kukidhi vigezo vifuatavyo:-

(i) Liwe na nafasi ya kutosha kuruhusu shughuli zote kufanyika kwa urahisi.

(ii) Liwe na mwanga na hewa ya kutosha kuruhusu mazingira mazuri na ubora wa vipodozi vilivyomo.

(iii) Liwe la kudumu na imara.

(iv) Liwe na paa na dari imara lisilovuja.

(v) Liwe na sakafu imara inayosafishika kwa urahisi.

(vi) Lisiwe na muingiliano na vyumba vingine ambavyo havina uhusiano na biashara ya vipodozi.

(vii) Lisiwe na mwingiliano wa moja kwa moja na nyumba au makazi ya watu.

(viii) Liwe na rafu za kutosha kutunzia makundi mbalimbali ya vipodozi.

4.2.3 **Ghala la kuhifadhia vipodozi**

a) Ghala la kuhifadhi vipodozi linapaswa kuwa katika mazingira safi na salama yasiyo hatarisha ubora wa vipodozi.

b) Ghala liwe katika eneo linalofikika kwa urahisi ili kurahisisha ukaguzi na ufuatiliaji.

c) Ghala litatakiwa kutumika kwa ajili ya kuhifadhia na sio kuuzia vipodozi.

d) Ghala la kuhifadhia vipodozi litapaswa kukidhi vigezo vifuatavyo:

(i) Liwe na nafasi ya kutosha kuhifadhi makundi mbalimbali ya bidhaa za vipodozi.

(ii) Liwe na mwanga wa wastani na hewa ya kutosha kuruhusu mazingira mazuri ya uhifadhi na usalama wa vipodozi vilivyomo.

(iii) Liwe na sakafu na kuta imara zinazosafishika kwa urahisi.

(iv) Liwe na dari imara lisilovuja.

(v) Lisiruhusu wanyama na wadudu waharibifu kuingia kwa urahisi.

(vi) Liwe na rafu au chaga za kuhifadhia vipodozi.

(vii) Lisiwe na muingiliano na nyumba ya makazi.

4.2.4 **Magari ya kubebea vipodozi**

a) Magari ya kubebea vipodozi yatakayosajiliwa ni yale yanayotumiwa na wenye viwanda na maduka ya jumla kusafirisha vipodozi.

b) Gari litatakiwa kukidhi vigezo vifuatavyo:-

(i) Liwe na nafasi ya kutosha kuhifadhi vipodozi.

(ii) Liwe na hewa ya kutosha kuruhusu mazingira mazuri ya usafirishaji.

(iii) Liwe safi wakati wote.

(iv) Lisiwe linavuja hasa wakati wa mvua au kuruhusu mwanga wa jua.

(v) Lisichorwe wala kubandikwa matangazo ambayo hayajaidhinishwa na TFDA.

SEHEMU YA TANO: USAJILI WA VIPODOZI

5.1 Pamoja na kusajili majengo, watengenezaji, waingizaji au wauzaji wa jumla watapaswa kusajili vipodozi vyao kabla ya kuruhusiwa kutumika nchini. Utaratibu wa usajili umeainishwa kwenye Mwongozo wa Usajili wa Vipodozi *(Guidelines for Submission of Documentation for Marketing Authorization of Cosmetic Products).*

5.2 Wafanyabiashara wengine watapaswa kuhifadhi na kuuza vipodozi ambavyo vimesajiliwa na TFDA. Orodha ya vipodozi vilivyosajiliwa inapatikana kwenye ofisi za TFDA makao makuu na kanda pamoja na tovuti ya TFDA www.tfda.go.tz

5.3 Waingizaji ambao wameshasajili vipodozi vyao TFDA wanaweza kuwaidhinisha wafanyabiashara wengine kuviingiza nchini. Waingizaji hao watapaswa kuwasilisha TFDA barua na makubaliano ya kisheria (*Power of attorney*).

5.4 Uingizaji wa vipodozi nchini utafuata utaratibu ulioainishwa kwenye Mwongozo wa Uingizaji na Utoaji Vipodozi Nje ya Nchi (*Guidelines for Importation and Exportation of Cosmetic Products*).

5.5 Viwanda vidogo havitaruhusiwa kutengeneza vipodozi vilivyoainishwa kwenye kundi la vipodozi maalum (*special cosmetics*) kwa mujibu wa Mwongozo wa Usajili wa Vipodozi.

5.6 Wale wote wanaofanya biashara ya vipodozi kwa kutumia mitandao watapaswa kuhakikisha vipodozi wanavyotangaza na kuuza vimesajiliwa na kupewa kibali na TFDA kama ambavyo imeainishwa kwenye mwongozo huu.

5.7 Mfanyabiashara hataruhusiwa kutumia nembo ya TFDA kwenye bidhaa au biashara yake.

SEHEMU YA SITA: MGAWANYO WA MAJUKUMU

6.1 TFDA Makao Makuu

a) Kuandaa kanuni na miongozo ya uendeshaji na usimamizi wa maeneo yanayojihusisha na biashara ya vipodozi.

b) Kupokea maombi, kufanya tathmini na kusajili vipodozi.

c) Kupokea maombi, kufanya tathmini na kuidhinisha matangazo ya vipodozi.

d) Kufanya ukaguzi kuhakiki utengenezaji bora wa vipodozi kwenye viwanda kama sehemu ya usajili.

e) Kutoa vibali vya uingizaji na utoaji nje ya nchi wa vipodozi.

f) Kushughulikia rufaa zote zinazohusisha vipodozi.

g) Kusimamia uondoaji na uteketezaji wa vipodozi visivyofaa kwa matumizi ya binadamu.

h) Kutoa elimu kwa wajasiriamali kuhusiana na masuala ya udhibiti wa vipodozi kwa kushirikiana na SIDO, VETA na TBS.

6.2 Ofisi za Kanda

a) Kupokea maombi, kufanya tathmini, kufanya utambuzi na kusajili maeneo yote yanayojihusisha na biashara ya vipodozi.

b) Kufanya ukaguzi wa maeneo yote yanayojihusisha na biashara ya vipodozi ikiwa ni pamoja na kubaini yale ambayo hayajasajiliwa.

c) Kufanya ukaguzi kwenye vituo vya forodha ili kuhakiki vibali vilivyotolewa Makao Makuu kabla ya kuruhusu vipodozi kuingia au kutoka nje ya nchi.

d) Kufanya ufuatiliaji wa matangazo yanayotolewa kwenye maeneo yanayozunguka kanda husika.

e) Kupokea na kushughulikia malalamiko ya wateja.

f) Kufanya kazi kwa kushirikiana na watendaji wengine wa Serikali ikiwa ni pamoja na Halmashauri, SIDO, VETA, TBS, Vyombo vya ulinzi na usalama na Mahakama.

g) Kutoa elimu kwa wajasiriamali na wadau wengine kuhusiana na udhibiti wa vipodozi kwenye kanda husika.

h) Kusimamia uondoaji na uteketezaji wa vipodozi visivyofaa kwa matumizi ya binadamu kwenye kanda husika.

SEHEMU YA SABA: UENDESHAJI WA BIASHARA YA VIPODOZI

7.1 Majukumu ya mmiliki na msimamizi wa biashara ya vipodozi

7.1.1 Mmiliki anatakiwa kuhakikisha kwamba:

a) Anahuisha kibali cha kiwanda au duka kabla ya tarehe 30 Juni ya kila mwaka.

b) Ana msimamizi ambaye ana sifa zilizoainishwa kwenye mwongozo huu.

c) Anatengeneza, kuuza au kuhifadhi vipodozi vilivyosajiliwa.

d) Kuna vitabu vya rejea na kumbukumbu mbalimbali kama zilivyoainishwa katika Mwongozo huu.

e) Vigezo vya kiwanda au duka la vipodozi vinazingatiwa muda wote.

7.1.2 Msimamizi au muuzaji anatakiwa kuhakikisha kwamba:

a) Anasimamia shughuli zote za kitaalamu kuhusu vipodozi.

b) Jengo lina kibali halali kutoka TFDA ambacho kimetundikwa sehemu ya wazi.

c) Nyaraka zilizopo zinajazwa ipasavyo na kutunza kumbukumbu mbalimbali ikiwemo kumbukumbu za manunuzi na mauzo.

d) Jengo la biashara linakuwa katika hali ya usafi muda wote.

7.2 Utunzaji wa vipodozi

7.2.1 Utunzaji mzuri wa vipodozi ni jukumu la msingi ili kuhakikisha vipodozi vinaendelea kuwa na viwango vya ubora na usalama.

7.2.2 Ubora na usalama wa vipodozi unaweza kuathiriwa na joto, mwanga, unyevunyevu au uchafu. Ili kuepuka athari hizo mmiliki na msimamizi kwa pamoja wana wajibu wa kuhakikisha kwamba:-

a) Vipodozi vinahifadhiwa katika sehemu safi, kavu, isiyo na joto kali, mwanga wa jua na kwa kuzingatia maelezo ya utunzaji kama yalivyoainishwa kwenye lebo.

b) Vipodozi vina vifungashio vyake vya asili muda wote.

c) Vipodozi vinapangwa kwenye rafu au chaga.

d) Vipodozi visivyofaa kwa matumizi vinatengewa sehemu maalum na kuainishwa kwa herufi kubwa **"SI KWA MATUMIZI".**

7.3 Uondoaji kwenye soko vipodozi visivyofaa kwa matumizi

7.3.1 Inaweza kutokea kuna vipodozi ambavyo vitahitajika kuondolewa kwenye soko kutokana na matatizo ya ubora au usalama.

7.3.2 Maelekezo ya kuondoa kutoka katika soko vipodozi visivyofaa kwa matumizi yanaweza kutoka kwa mtengenezaji wa vipodozi husika, msambazaji au TFDA.

7.3.3 Mmiliki atatakiwa kuwa na uwezo wa kuondoa kutoka katika soko vipodozi visivyofaa kwa haraka.

7.3.4 Mmiliki atapaswa kutoa ushirikiano kwa TFDA ili kufanikisha uondoaji wa vipodozi visivyofaa kwa haraka na ufanisi ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa ya kila hatua ya uondoaji.

7.3.5 Zoezi la kuondoa vipodozi visivyofaa litafanyika mpaka ngazi ya duka la rejareja.

7.4 Uteketezaji wa vipodozi visivyofaa kwa matumizi

7.4.1 Vipodozi visivyofaa kwa matumizi visiteketezwe kiholela.

7.4.2 Mmiliki au msimamizi wa biashara atatakiwa kuwasiliana na Ofisi ya kanda ya TFDA kupata utaratibu wa kuteketeza vipodozi visivyofaa kwa matumizi.

7.4.3 Zoezi la uteketezaji litafanyika chini ya uangalizi wa wakaguzi wa TFDA na wawakilishi kutoka Taasisi nyingine za Serikali.

7.5 Utunzaji wa kumbukumbu na vitabu vya rejea

7.5.1 Msimamizi wa kiwanda au duka la kipodozi lililosajiliwa atapaswa kujaza na kuweka kumbukumbu sahihi zinazohusu uendeshaji wa biashara kama orodha ya vipodozi vinavyotengenezwa au kuuzwa, vipodozi visivyofaa kwa matumizi, kumbukumbu za manunuzi na mauzo n.k.

7.5.2 Vile vile atatakiwa kuwa na vitabu mbalimbali vya rejea ili kurahisisha utendaji wa kazi kama vile mwongozo wa kuwatambua na kuwasajili wajasiriamali wa vipodozi, kanuni za udhibiti wa vipodozi na Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sura 219 na Orodha ya vipodozi vilivyosajiliwa na TFDA.

7.6 Mabadiliko katika uendeshaji wa biashara

7.6.1 Badiliko lolote linalohusu kiwanda cha kutengeneza vipodozi au duka la kuuza vipodozi na ghala ikiwa ni pamoja na kubadili mmiliki, msimamizi, jengo, eneo na jina la biashara linatakiwa kufuata utaratibu ufuatao:-

a) Mmiliki atoe taarifa ya mabadiliko husika kwenye Ofisi za kanda kwa barua.

b) Badiliko linalohusu jengo au eneo la biashara, mmiliki atawajibika kuomba upya kusajili kiwanda au duka katika jengo au eneo jingine kwa kufuata taratibu za maombi kama zilivyoainishwa katika mwongozo huu. Mmiliki atatakiwa kurudisha TFDA cheti cha usajili na kibali kilichotolewa awali.

7.7 Uhuishaji wa kibali cha kutengeneza au kuuza vipodozi

7.7.1 Kwa mujibu wa Sheria, kibali cha kuendesha kiwanda au duka la vipodozi au ghala kinafikia ukomo tarehe 30 Juni ya kila mwaka. Hivyo basi mmiliki wa kiwanda au duka la vipodozi ana wajibu wa kuhakikisha yafuatayo: -

a) Anawasilisha maombi na kulipia ada ya kuhuisha kibali miezi mitatu (3) kabla ya muda wa ukomo.

b) Mmiliki atajaza fomu ya kuomba kibali na kuwasilisha ofisi ya kanda kama ilivyoainishwa kwenye mwongozo huu.

c) Mmiliki atakayechelewa kuhuisha kibali chake atawajibika kulipa faini ya asilimia 25 ya ada ya kibali kwa mujibu wa Kanuni za Ada na Tozo za TFDA.

7.8 Kusitisha biashara

7.8.1 Mmiliki wa kiwanda au duka la vipodozi anaweza kusitisha biashara:-

a) Kwa hiari yake.

b) Kwa amri ya TFDA au Mahakama.

7.8.2 Endapo biashara itasitishwa, TFDA itatoa siku tisini (90) ili taratibu za kuondoa vipodozi zikamilishwe kwa mujibu wa Sheria kabla ya kibali kusitishwa rasmi.

7.9 Makosa na adhabu zinazohusiana na uvunjaji wa Sheria na Kanuni

Ukiukwaji na uvunjaji wa Sheria na Kanuni zinazosimamia uendeshaji wa biashara ya vipodozi utaenda sambamba na makosa na adhabu zilizoainishwa katika Sheria ya

Chakula, Dawa na Vipodozi, Sura 219 na Kanuni za Udhibiti wa Vipodozi za mwaka 2010.

7.10 Ukataji wa rufaa

7.10.1 Mmiliki au msimamizi asiyeridhika na maamuzi yoyote ya TFDA atafuata utaratibu ufuatao:-

a) Kuwasilisha rufaa ya maandishi ya kutoridhishwa na maamuzi kwa Mkurugenzi Mkuu TFDA ndani ya siku sitini (60) ili aweze kupitia upya.

b) Ikiwa Mkurugenzi Mkuu hataridhika na rufaa iliyowasilishwa, maamuzi ya awali yatabakia.

c) Endapo mmliki au msimamizi hataridhika na mapitio ya Mkurugenzi Mkuu, atakata rufaa kwa Waziri mwenye dhamana ya afya ndani ya siku thelathini (30) tangu siku ya maamuzi.

d) Maamuzi ya Waziri mwenye dhamana ya afya yatakuwa ndio ya mwisho.

SEHEMU YA NANE: VIAMBATISHO

Kiambatisho 1: Fomu ya utambuzi wa wajasiriamali wadogo wa vipodozi

TFDA Tanzania Food & Drugs Authority	**FOMU YA KUTAMBUA WAJASIRIAMALI WANAOJIHUSISHA NA UTENGENEZAJI NA UUZAJI WA VIPODOZI**	**TFDA/DMC/CCM/F/..** **Rev 0**

Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Chakula na Dawa,
P. O. Box 77150,
Dar es Salaam

SEHEMU A: TAARIFA ZA MJASIRIAMALI

1. Jina la mmiliki:
   .....
2. Jina la kampuni/biashara:
   .....
3. Anwani ya kampuni/biashara:
   .....

Sanduku la posta	Namba ya simu	Barua pepe
.....	.....	.....

4. Eneo biashara ilipo

Namba ya kiwanja	Namba ya kitalu	Namba ya nyumba
.....	.....	.....
Mtaa	Kata	Wilaya
.....	.....	.....
Mkoa		
.....		

5. Jina la Msimamizi wa kampuni/ biashara | Namba ya simu: | Barua pepe

.....	.....	.....

SEHEMU B: TAARIFA ZA BIASHARA

Weka alama ya √ kwenye sanduku sahihi

1. Aina ya biashara

Kutengeneza ☐ Kuuza ☐ Nyingine ☐

Kama Nyingine (Eleza)

.....

2. Kama ni mtengenezaji, ainisha aina ya vipodozi unavyotengeneza:-

Na.	Jina na aina ya kipodozi (mf. sabuni, losheni, krimu, shampoo nk.)	Orodha ya viambato vilivyomo	Kiasi kinatengenezwa kwa mkupuo mmoja (lita, vipande, miche)	Matumizi

(Tumia karatasi ya ziada inapobidi)

SEHEMU C: GHARAMA YA UWEKEZAJI

1. Kiasi cha mtaji wa uendeshaji (kwa shilingi)
   .....
2. Makadirio ya jumla ya mtaji wa mashine na vifaa vya kutengeneza vipodozi (kwa shilingi)
   .....
3. Idadi ya wafanyakazi waliopo
   .....

SEHEMU D: USAJILI WA BIASHARA NA TARATIBU NYINGINE

1. Biashara imesajiliwa na BRELA? Ndiyo ☐ Hapana ☐
2. Biashara imesajiliwa na TFDA? Ndiyo ☐ Hapana ☐
3. Kama ndiyo taja namba ya usajili
   .....
4. Vipodozi vimesajiliwa na TFDA? Ndiyo ☐ Hapana ☐ Sijui ☐
5. Viwango vya ubora wa vipodozi umethibitishwa na TBS? Ndiyo ☐ Hapana ☐ Sijui ☐
6. Biashara ina leseni kutoka Halmashauri husika? Ndiyo ☐ Hapana ☐
7. Biashara imepata namba ya mlipa kodi? Ndiyo ☐ Hapana ☐

   **Kwa 1-5 kama jibu ni ndio, weka nakala ya nyaraka husika.

8. Biashara imekuwa ikipata huduma kutoka SIDO? Ndiyo ☐ Hapana ☐

Kama jibu ni ndio, taja huduma ulizo pata

.....

.....

SEHEMU E: UTHIBITISHO WA MJASIRIAMALI

Mimi ..... nikiwa kama ..... (taja cheo/nafasi katika kampuni/biashara) nathibitisha kwamba maelezo yaliyotolewa katika fomu hii ni ya kweli na sahihi.

Saini: ..... Tarehe: .....

Muhuri: .....

SEHEMU E: KWA MATUMIZI YA OFISI TU

1. Jina na saini ya Afisa aliyepokea: ..... Tarehe: .....
   Muhuri wa ofisi: .....

2. **Maoni kuhusu biashara**

   .....

   .....

   Jina na saini ya Meneja anayehusika..... Tarehe.....

Kiambatisho 2: Fomu ya maombi ya usajili wa jengo (kwa kiswahili)

TFDA Tanzania Food & Drugs Authority	**FOMU YA MAOMBI YA USAJILI WA JENGO**	**TFDA/DMC/CCM/F/.. Rev 0**

Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Chakula na Dawa,
P. O. Box 77150,
Dar es Salaam

SEHEMU A: TAARIFA ZA MWOMBAJI

Ninaomba/Tunaomba kupatiwa usajili wa jengo jipya kwa mujibu wa Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya mwaka 2003.

1. Jina la mwombaji.....

2. Anuani ya posta..... Namba ya simu .....

   Faksi..... Barua pepe .....

3. Jina kamili la Mbia na Mkurugenzi/Wakurugenzi .....

   .....

4. Mahali jengo lilipo/namba ya kiwanja .....

   Mtaa /Kijiji/Kata.....Wilaya/Manispaa/Jiji .....

5. Jengo linaombewa usajili kwa ajili ya biashara ya .....

6. Biashara husika itakuwa chini ya usimamizi wa mtaalamu, Mr /Ms /Mrs. /Dr. /Prof (taja Jina kamili).....ambaye ni mtaalamu wa ..... (Ambatisha nakala ya cheti)

7. Jina la jengo .....

8. Endapo nitapatiwa usajili wa jengo nitaliweka katika hali ya usafi kwa mujibu wa matakwa ya Sheria tajwa, Kanuni na Miongozo husika.

9. Sijawahi/ Hatujawahi kutenda kosa lolote kuhusiana na Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sura 219.

   Kumbuka: Uthibitisho wa uongo ni kosa la jinai

   Tarehe..... Saini ya mwombaji .....

SEHEMU B: MAONI YA MKAGUZI WA HALMASHAURI/ MKOA/MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA (futa kisichohitajika)

Mimi, Bw. /Bi./Dk./Prof..... mkaguzi wa Halmashauri/ Mkoa/Mamlaka ya Chakula na Dawa wa (taja anuani ya posta) .....nathibitisha kwamba nimekagua jengo lililotajwa hapo juu na nathibitisha kwamba **linakidhi/halikidhi** vigezo vya usajili wa jengo.

Tafadhali toa sababu za kutokidhi .....

.....

.....

Jina la Mkaguzi	Saini na muhuri	Tarehe
1.	.....	.....
2.....	.....	.....

KWA MATUMIZI YA OFISI TU

Ada Tshs.....Namba ya risiti ..... ya tarehe .....

Usajili umetolewa/haujatolewa kwa sababu .....

Namba ya usajili ..... Imethibitishwa na .....

....
Tarehe Muhuri na Saini ya Mkurugenzi Mkuu

Kiambatisho 3: Fomu ya maombi ya kibali/ leseni ya biashara (kwa kiswahili)

TFDA Tanzania Food & Drugs Authority	**FOMU YA MAOMBI YA KIBALI**	**TFDA/DMC/CCM/F/..** **Rev 0**

Mkurugenzi mkuu,
Mamlaka ya Chakula na Dawa,
P. O. Box 77150,
Dar es Salaam

SEHEMU I: TAARIFA ZA MWOMBAJI

Ninaomba/ Tunaomba kupatiwa kibali kipya cha kutengeneza, kuuza, kufungasha, kuhifadhi, kusambaza ifuatavyo: .....

1. Jina la mwombaji.....

2. Anuani ya posta..... Namba ya simu .....

   Faksi..... Barua pepe .....

3. Jina kamili la Mbia na Mkurugenzi/Wakurugenzi
   .....

4. Mahali jengo lilipo/namba ya kiwanja
   .....

   Mtaa /Kijiji/Kata.....Wilaya/Manispaa/Jiji .....

5. Namba ya usajili wa jengo ..... ya mwaka .....

6. Namba ya kibali cha sasa ..... cha tarehe ..... tarehe ya mwisho wa matumizi .....

SEHEMU II: KWA MTENGENEZAJI TU

TAARIFA YA USAJILI WA BIDHAA

Natarajia kutengeneza bidhaa zifuatazo ambazo taarifa zake za usajili zimeelezwa hapa chini:

Na.	**Jina la bidhaa**	**Jina la kibiashara**	**Namba ya usajili**	**Kwa matumizi ya ofisi tu**

(Tumia karatasi ya ziada inapobidi)

SEHEMU III: UTHIBITISHO WA MWOMBAJI

1. Endapo nitapatiwa kibali nitaliweka jengo la biashara katika hali ya usafi kwa mujibu wa matakwa ya Sheria tajwa, Kanuni na Miongozo husika.

2. Sijawahi/ Hatujawahi kutenda kosa lolote kuhusiana na Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sura 219.

Kumbuka: Uthibitisho wa uongo ni kosa la jinai.

Tarehe …… ……
Saini ya mwombaji na muhuri

KWA MATUMIZI YA OFISI TU

Ada Tshs……Namba ya risiti …… ya tarehe ……

Kibali kimetolewa/hakijatolewa kwa sababu
……

Namba ya Kibali …… Imethibitishwa na ……

…… ……
Tarehe Muhuri na Saini ya Mkurugenzi Mkuu

Kiambatisho 4: Fomu ya ukaguzi wa kiwanda kidogo cha vipodozi

TFDA Tanzania Food & Drugs Authority	**FOMU YA UKAGUZI WA KIWANDA KIDOGO CHA KUTENGENEZA VIPODOZI**	**TFDA/DMC/CCM/F/.. Rev 0**

SEHEMU A: TAARIFA ZA KIWANDA

Jina la Kiwanda/Biashara	Mtaa/Kijiji	Kata	Wilaya na Mkoa
Jina la Mmiliki		Namba za simu..... Barua pepe.....	
Jina la Msimamizi/Mtaalam ..... Taaluma ya Msimamizi		Namba za simu..... Barua pepe.....	
Namba ya usajili wa jengo ..... ya mwaka ..... Namba ya kibali ..... cha mwaka ..... tarehe ya mwisho wa matumizi			

SEHEMU B: AINA NA TAREHE YA UKAGUZI

Dhumuni la ukaguzi (usajili/ kawaida/ufuatiliaji/malalamiko (futa kisichohitajika)/ Mengine (taja) .....

Tarehe ..... Muda .....

SEHEMU C: TAARIFA YA UKAGUZI

Na.	**Hali ya Kiwanda**	**Alama**		**Maelezo ya ziada**
1.0	**Mahali**			
1.1	Mazingira safi na salama yasiyohatarisha ubora na usalama wa vipodozi vinavyotengezwa mfano hakuna hewa chafu, vumbi, moshi wenye sumu n.k	2		
1.2	Eneo linafikika kwa urahisi na katika misimu yote ya mwaka.	1		
2.0	**Jengo**			
2.1	Jengo ni imara na la kudumu	1		
2.2	Kuna nafasi ya kutosha kuruhusu • uwekaji wa vifaa • utengenezaji	5		

Na.	Hali ya Kiwanda	Alama		Maelezo ya ziada
	• uhifadhi wa malighafi na vipodozi, vilivyotengenezwa • uchunguzi wa vipodozi • kazi kufanyika kwa mpangilio mzuri			
2.3	Kuna mwanga na hewa ya kutosha	1		
2.4	Dari imara na halivuji	1		
2.5	Kuta na sakafu imara, nyororo, hazina mipasuko, safi na zinasafishika au kukarabatiwa kwa urahisi.	1		
2.6	Hakuna muingiliano na vyumba vingine au makazi ambayo yanasababisha uchafuzi wa bidhaa zinazotengenezwa	2		
2.7	Lina vifaa vya kuzuia/Haliruhusu wanyama au wadudu waharibifu kuingia	1		
2.8	Lina rafu/ chaga za kuhifadhi malighafi na vipodozi vilivyotengenezwa	1		
3.0	**Vifaa vya kutengeneza**			
3.1	Vifaa vinatosha kukidhi mahitaji	1		
3.2	Vifaa havina mikwaruzo ya kuweza kuhifadhi uchafu, kemikali au wadudu	1		
3.3	Vifaa vinasafishika kirahisi, havishiki kutu, havichubuki wala kusababisha uchafuzi wa bidhaa inayotengenezwa	2		
3.4	Vifaa vinaruhusu usafi kufanyika kuondoa mabaki ya bidhaa iliyopita	2		
3.5	Vifaa vinatunzwa vizuri katika hali ya usafi	1		
4.0	**Malighafi**			
4.1	Malighafi zinatoka kwenye vyanzo halali	2		
4.2	Malighafi zinatunzwa katika hali ya usafi	1		
4.3	Maji safi na salama	1		
5.0	**Wafanyakazi**			
5.1	Kuna wafanyakazi wa kutosha kukidhi mahitaji	1		
5.2	Kuna msimamizi mtaalamu wa shughuli za uzalishaji	1		
5.3	Wafanyakazi wamepata mafunzo ya utengenezaji bora wa vipodozi	2		
5.4	Wafanyakazi wana mavazi na vifaa maalum vya kujikinga wakati wa uzalishaji	1		
5.5	Wafanyakazi ni wasafi muda wote wa uzalishaji	1		
6.0	**Usafi wa Mazingira**			
6.1	Kuna vyoo vya kutosha kwa ajili ya wafanyakazi	1		

Na.	Hali ya Kiwanda	Alama		Maelezo ya ziada
6.2	Kuna maji ya kutosha kwa ajili ya uzalishaji na usafi kwa ujumla	1		
6.3	Kuna eneo maalumu la kunawia mikono pamoja na sabuni au kipukusi	1		
6.4	Kuna utaratibu maalum wa kuhifadhi na kuharibu taka	2		
6.5	Hakuna uwezekanao wa kuchafua mazingira yanayozunguka	2		
7.0	**Vitabu vya rejea na kumbukumbu**			
7.1	Kuna vyeti vya elimu na ujuzi wa wafanyakazi	1		
7.2	Kuna kumbukumbu za mafunzo ya wafanyakazi	1		
7.3	Kuna kumbukumbu za usafi	1		
7.4	Kuna kumbukumbu za manunuzi ya malighafi na mauzo ya vipodozi	1		
7.5	Kuna kitabu cha kumbukumbu za ukaguzi	1		
7.6	Kuna kumbukumbu ya bidhaa zilizozalishwa	1		
7.7	Kuna kumbukumbu za malalamiko ya ubora na usalama wa bidhaa	1		
7.8	Kuna kumbukumbu za uchunguzi wa bidhaa	1		
7.9	Kuna kumbukumbu za bidhaa zisizofaa/zilizorejeshwa kutoka kwenye soko	1		
7.10	Kuna Kanuni, miongozo mbalimbali yaTFDA na vitabu vya rejea	1		
JUMLA YA ALAMA (1.1 HADI 7.10)		**50**		
UTEKELEZAJI				
• Kiwanda kilichopata alama 90 hadi 100 litasajiliwa na kupewa kibali				
• Kiwanda kilichopata alama 75 hadi 89 litapewa miezi mitatu kusahihisha upungufu uliojitokeza				
• Kiwanda kilichopata alama 74 na kushuka chini litafungiwa kwa mujibu wa Sheria				

SEHEMU D: MAONI YA MKAGUZI

Mimi/Sisi ..... Mkaguzi / Wakaguzi wa TFDA nimekagua/ tumekagua jengo la kiwanda hiki na alama zilizowekwa hapo juu ni za kweli. Ninatambua/ tunatambua kuwa utoaji wa taarifa za uwongo/zisizo sahihi kutapelekea mimi/sisi kuchukuliwa hatua za kinidhamu na mwajiri.

Saini za wakaguzi Tarehe

1. ....
2. ....

SEHEMU E: UTHIBITISHO WA MMILIKI/ MSIMAMIZI WA KIWANDA/ BIASHARA

Mimi ..... nathibitisha kwamba jengo la kiwanda changu limekaguliwa na wakaguzi na alama zilizowekwa ni za kweli.

Saini ya Mmiliki/ Msimamizi ..... Tarehe: .....

Kiambatisho 5: Cheti cha usajili wa jengo

TANZANIA FOOD AND DRUGS AUTHORITY

REGISTRATION CERTIFICATE OF PREMISES
Made under Section 21(3) of the Tanzania Food, Drugs and Cosmetics Act, 2003

This is to certify that the premises owned by M/S ..... of P. O. Box ..... located at ..... in ..... District/Municipal in ..... region have been registered to be used as ..... for ..... with premises Registration Number .....

Subject to the following conditions:-

1. The premises and the manner in which the business is to be conducted must conform to requirements of the Tanzania Food, Drugs and Cosmetics Act, 2003 or any other written law related to the premises registration at all times failing of which this certificate shall be suspended or revoked.

2. Any change in the ownership, business name and location of the registered premises shall be approved by the Authority.

3. This certificate is not transferable to other premises or to any other person.

4. This certificate shall be displayed conspicuously in the registered premises.

.....
DATE

.....
DIRECTOR GENERAL

Kiambatisho 6: Kibali/ leseni ya biashara

TANZANIA FOOD AND DRUGS AUTHORITY

BUSINESS PERMIT

Made under Section 21(3) of the Tanzania Food, Drugs and Cosmetics Act, 2003

Permit No .....

Permit is hereby granted to M/S ..... of P. O. Box ..... to operate a business of ..... at the premises situated/lying between ..... in ..... District/Municipality in ..... region having Registration No. .....

This Permit shall have and continue to have effect from and including the day when it is issued until it ceases to have effect on 30th June .....

Issued on ..... Fees paid Tshs .....

Receipt No .....

.....

DATE

.....

DIRECTOR GENERAL

CONDITIONS

1. This Permit does not authorize the holder to operate business in unregistered premises or during the period of suspension, revocation or cancellation of registration of the premises in respect of which it was issued.

2. This Permit is not transferable without a written approval of the Authority.

Kiambatisho 7: Fomu ya ukaguzi wa duka/ghala la kuhifadhia vipodozi

TFDA Tanzania Food & Drugs Authority	**FOMU YA UKAGUZI WA DUKA/GHALA LA KUHIFADHI VIPODOZI**	**TFDA/DMC/CCM/F/.. Rev 0**

SEHEMU A: TAARIFA ZA DUKA/GHALA

Jina la Duka /Biashara	Mtaa/Kijiji	Kata	Wilaya na Mkoa
Jina la Mmiliki wa Duka/Biashara		Namba za simu…… Barua pepe ……	
Jina la Msimamizi ……		Namba za simu…… Barua pepe ……	
Aina ya Biashara (**Duka la jumla/ Duka la jumla na rejareja/ Duka la rejareja/ ghala** (Futa isiyo sahihi)			
Namba ya usajili wa jengo …… ya mwaka …… Namba ya kibali …… cha mwaka …… tarehe ya mwisho wa matumizi ……			
Jina na muuzaji/ wauzaji …… Elimu ……			

SEHEMU B: AINA NA TAREHE YA UKAGUZI

Dhumuni la ukaguzi (usajili/ kawaida/ufuatiliaji/malalamiko (futa kisichohitajika)/ Mengine (taja) ……

Tarehe …… Muda ……

SEHEMU C: TAARIFA YA UKAGUZI

Na.	**Hali ya Duka/Ghala**	**Alama**		**Maelezo ya ziada**
1.0	**Mahali**			
1.1	Eneo lina mazingira safi na salama yasiyohatarisha ubora wa vipodozi	3		
1.2	Eneo linafikika kwa urahisi na katika misimu yote ya mwaka	2		
2.0	**Jengo**			
2.1	Jengo ni imara na la kudumu	2		
2.2	Lina nafasi ya kutosha kuruhusu shughuli kufanyika kwa urahisi au kuhifadhi makundi mbalimbali ya	3		

Na.	Hali ya Duka/Ghala	Alama		Maelezo ya ziada
	vipodozi			
2.3	Lina mwanga na hewa ya kutosha	2		
2.4	Lina paa na dari imara na lisilovuja	2		
2.5	Lina kuta na sakafu imara zinazosafishika kwa urahisi.	2		
2.6	Halina muingiliano na vyumba vingine au makazi ambayo hayana uhusiano na biashara ya vipodozi	3		
2.7	Haliruhusu wanyama au wadudu waharibifu kuingia	2		
2.8	Lina rafu au chaga za kutosha kutunzia vipodozi	2		
2.9	Ghala linatumika kuhifadhia na si kuuzia	2		
3.0	**Muuzaji na vyeti vyeti vya usajili**			
3.1	Kuna muuzaji mwenye sifa zinazokubalika	2		
3.2	Kuna vibali na vyeti vya usajili vimetundikwa	2		
4.0	**Vitabu vya rejea na kumbukumbu**			
4.1	Kuna kumbukumbu za manunuzi na mauzo ya vipodozi	3		
4.2	Kuna kitabu cha kumbukumbu za ukaguzi	2		
4.3	Kuna kumbukumbu za bidhaa zisizofaa/zilizorejeshwa kutoka kwenye soko	2		
4.4	Kuna orodha ya vipodozi vilivyosajiliwa	2		
4.5	Kuna Kanuni, miongozo mbalimbali yaTFDA na vitabu vya rejea	2		
JUMLA YA ALAMA (1.1 HADI 4.5)		**40**		
UTEKELEZAJI				
• Kiwanda kilichopata alama 90 hadi 100 litasajiliwa na kupewa kibali				
• Kiwanda kilichopata alama 75 hadi 89 litapewa miezi mitatu kusahihisha upungufu uliojitokeza				
• Kiwanda kilichopata alama 74 na kushuka chini litafungiwa kwa mujibu wa Sheria				

SEHEMU D: MAONI YA MKAGUZI

Mimi/Sisi ..... Mkaguzi / Wakaguzi wa TFDA nimekagua/ tumekagua jengo la duka/ghala hili na alama zilizowekwa hapo juu ni za kweli. Ninatambua/ tunatambua kuwa utoaji wa taarifa za uwongo/zisizo sahihi kutapelekea mimi/sisi kuchukuliwa hatua za kinidhamu na mwajiri.

Saini za wakaguzi Tarehe

1. ....
2. ....

SEHEMU E: UTHIBITISHO WA MMILIKI/ MSIMAMIZI WA DUKA/GHALA

Mimi ..... nathibitisha kwamba jengo la duka/ghala langu limekaguliwa na wakaguzi na alama zilizowekwa ni za kweli.

Saini ya Mmiliki/ Msimamizi ..... Tarehe: .....

Haki zote zimehifadhiwa:
Nyaraka hii inadhibitiwa, hairuhusiwi kunakili bila ya idhini ya Meneja wa Uhakiki Mifumo au Mkurugenzi wa Dawa na Bidhaa Nyongeza au Mkurugenzi Mkuu.
Nyaraka halisi au nakala iliyoidhinishwa ndiyo itakayotumika.